**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO KWENYE KONGAMANO KUHUSU "USIMAMIZI BORA WA FUKWE KWA MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII NCHINI TANZANIA"

**HOTELI YA MALAIKA BEACH RESORT, MWANZA**
**TAREHE 23 NOVEMBA, 2022**

***Mhe. Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;***

***Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***

***Mhe. Mary Masanja (Mb), Naibu Waziri Wa Maliasili na Utalii;***

***Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza;***

***Ndugu. Reuben Sixbert Jichabu, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Mwanza na Viongozi wote wa Chama mliopo;***

***Bw. Kadari Singo, Afisa Mtendaji Mkuu, Taasisi ya UONGOZI;***

***Mstahiki Meya, Manispaa ya Nyamagana na Manispaa ya Ilemela;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***

***Viongozi wa Serikali, Mashirika ya Umma na Binafsi Tanzania Bara na Zanzibar;***

***Viongozi na wawakilishi wa Wadau wa Maendeleo;***

***Viongozi wa Dini;***

***Wawakilishi wa vyama vya Siasa na Asasi zisizo za Kiserikali;***

***Watoa Mada na Wanajopo;***

***Waandishi wa Habari;***

***Wageni Waalikwa, Mabibi Na Mabwana***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

**Kwanza** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika salama hapa jijini Mwanza. **Pili**, napenda kuwashukuru sana wana Mwanza wakiongozwa na Kaimu Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee kwa mapokezi mazuri na kwa kukubali kuwa mwenyeji wa Kongamano hili muhimu sana kwa Taifa letu. **Tatu**, napenda kuishukuru Taasisi ya UONGOZI kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa mlezi wa Jukwaa hili la ukuaji wa kijani yaani *Green Growth Platform (GGP)*, na vilevile kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi kwenye Kongamano la mwaka huu, 2022. Nawapongeza sana ninyi pamoja na Manispaa ya jiji la Mwanza kwa matayarisho mazuri na kwa uamuzi wenu wa kufanya Jukwaa na kongamano hili katika Hoteli hii ya Malaika ambayo inaonesha kiuhalisia moja ya faida ya uwekezaji katika fukwe. **Hongereni sana!**

Kipekee kabisa, napenda pia kuwashukuru washiriki wote kwa kutenga muda wenu na kujitokeza kwa wingi ili kujadili masuala muhimu yanayohusu uwekezaji katika fukwe zetu na utunzaji wa mazingira kwa ujumla. Nimepewa taarifa kuwa majadiliano haya yatafanyika kinadharia na pia kwa vitendo pale mtakapotembelea mradi wa Tampere. Naamini ujuzi na uzoefu wenu kuhusu yale yatakayojadiliwa ni hazina kubwa kwetu na itasaidia Serikali kutekeleza jukumu lake la msingi la kujenga uchumi endelevu kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya 2025.

***Waheshimiwa Viongozi, Washiriki, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

Kama ambavyo tayari imeelezwa, Kongamano hili ni sehemu ya Jukwaa la Maendeleo Endelevu na lengo lake kuu ni kuhamasisha maendeleo jumuishi na endelevu yanayozingatia utunzaji mzuri wa mazingira na matumizi bora ya rasilimali kwa manufaa ya vizazi vya sasa na baadaye. Hivyo, kupitia Jukwaa hili tunapata fursa ya kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu kuhusu matumizi bora ya rasilimali zetu. Natambua kwamba Jukwaa hili hufanyika kila mwaka, ambapo kunakuwa na mada mbalimbali zinazolenga kujadili masuala yenye umuhimu kwa uchumi na mazingira ya Taifa letu. Nimevutiwa sana na mada kuu ya Kongamano la mwaka huu inayosema **"Usimamizi Bora wa Fukwe kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii nchini Tanzania."** Mada hii inalenga kubadilishana mawazo na mitazamo yetu juu ya namna bora ya kuwekeza kwenye fukwe zetu za bahari, maziwa na mito ili kutuletea faida za kiuchumi na kukuza mchango wake katika pato la Taifa na maendeleo kwa ujumla. Mada hii imekuja wakati mwafaka kwani hivi sasa kama Taifa tumeweka mkazo kuendeleza Uchumi wa Buluu. Hatuna budi kuchangamka na kuwa wabunifu kwenye suala hili (proactive and innovative). Lazima sisi viongozi, wataalamu na wawekezaji tujadili kwa pamoja namna bora ya kutunza, kusimamia na kuwekeza katika rasilimali hii adhimu ili kuongeza mchango wake kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Ni matumaini yangu kwamba mjadala katika kongamano hili utakuwa motomoto na kuja na mapendekezo ambayo yataleta mabadiliko chanya.

***Ndugu Washiriki;***

Tanzania ni nchi ya kipekee iliyopendelewa sana na Mwenyezi Mungu. Nchi yetu imezungukwa na maji pande zote na kujaliwa kuwa na bahari ya Hindi, maziwa makubwa kama Victoria, Tanganyika, Rukwa na Nyasa pamoja na mito ya kudumu. Uwepo wa bahari ya Hindi na maziwa umefanya nchi kuwa na fukwe nyingi na za kuvutia katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara na kule visiwani Zanzibar. Tumebarikiwa kuwa na zaidi ya kilomita 1400 za

ukanda wa Pwani ya bahari na fukwe safi, hifadhi 3 za baharini (*marine parks*) na maeneo tengefu ya baharini 15 (*marine reserves*). Aidha, maziwa na mito mikubwa kwa pamoja inaongeza idadi kubwa ya fukwe tulizonazo. Hata hivyo, pamoja na upendeleo huu tuliopewa na Mwenyezi Mungu, bado hatujaweza kutumia kikamilifu fukwe hizi kwa ajili ya maendeleo kama ilivyo katika nchi nyingine. Ni ukweli kwamba asilimia kubwa ya fukwe zetu hazijaendelezwa na zinakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa mazingira. Uharibifu huu unatokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu kando ya fukwe zetu kama vile uchimbaji wa mchanga, utupaji hovyo wa taka-maji na taka-ngumu, ujenzi holela, uvuvi haramu, kilimo na ufugaji holela, n.k. Athari hizi zimeonekana zaidi kando kando ya mito na kwenye fukwe za maziwa makubwa kama Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika. Aidha, mmomonyoko wa udongo kando ya fukwe umeripotiwa kuongezeka siku hadi siku katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Lindi, Pwani pamoja na visiwa vya Zanzibar. Ni dhahiri kuwa, tukiendelea na tabia hizi na tusipokuwa na mipango ya kuhakikisha usimamizi mzuri na uwekezaji sahihi, fukwe zetu zitatokomea na kumezwa na maji. Hivyo niwasihi sana viongozi, wataalam, wadau mbalimbali na watanzania wote kwa ujumla kila mmoja kwa nafasi yake, tufanye kila linalowezekana kuzinusuru fukwe zetu. Tuwe na mijadala mipana ambayo itachangia kuleta mabadiliko chanya na kusaidia Serikali kuimarisha mifumo yake ya kisera, kisheria na Kitaasisi ili kuweza kuboresha misingi ya usimamizi, utunzaji na uwekezaji bora kwenye fukwe zetu.

***Ndugu Washiriki;***

Suala la hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali ya Awamu ya Sita. Vilevile, dhamira ya Serikali ni kuharakisha maendeleo endelevu ya Taifa letu kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inayolenga kufikia uchumi jumushi wa Taifa lenye kipato cha kati na maisha bora kwa kila Mtanzania. Vilevile, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano pamoja na mikakati mingine ya kisekta na Ilani ya Uchanguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) vyote vimelenga kuiwezesha sekta binafsi kuwa kichocheo cha kukuza uchumi wa Taifa na kuleta maendeleo kwa watanzania. Aidha, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kuvutia wawekezaji na kuitangaza nchi yetu kupitia Filamu ya Royal Tour inayoonesha vivutio na fursa za uwekezaji zilizopo hapa nchini ikiwemo uwekezaji katika fukwe zetu. Hatuna budi kuunga mkono juhudi hizi, kushirikiana na kutumia fursa zilizopo ili Taifa letu liweze kusonga mbele haraka kimaendeleo. Suala la utunzaji, usimamizi na uwekezaji katika fukwe sio geni duniani hususan katika baadhi ya nchi za Afrika. Tuna mifano mingi mizuri ya uwekezaji wenye tija katika

fukwe ambao umeleta faida kubwa katika nchi hizo. Fursa katika eneo hili ni nyingi mno hususan kwenye sekta ya utalii. Kwa uzoefu wa nchi nyingine, uwekezaji kwenye fukwe unaweza kujumuisha ujenzi wa hoteli za kifahari (nyota 5), maduka makubwa (*mega shopping malls*), migahawa, masoko ya kitamaduni, viwanja vya michezo na fursa nyingine nyingi. Hivyo, napenda nitoe rai kwa wafanyabiashara, wadau na sekta binafsi kwa ujumla kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye fukwe zetu ili kutoa huduma zote muhimu sambamba na kuzalisha ajira kwa watanzania.

***Ndugu Viongozi na Washiriki;***
Nimeelezwa kuwa mtapata fursa ya kutembelea mradi wa Tampere unaolenga kufanya uwekezaji mkubwa wa fukwe hapa Jijini Mwanza. Ni matumaini yangu kuwa mtakapotembelea mradi huo mtajifunza kwa vitendo na kupata uelewa wa kutosha wa namna ya kuwekeza, kuendesha na kusimamia miradi ya aina hii. Nina hakika aina ya uwekezaji unaotarajiwa kufanyika hapo unaweza pia kufanyika hata kwenye maeneo ambayo hakuna fukwe. Aidha, tumeshuhudia nchi za wenzetu nyingi ambazo zilikuwa jangwa lakini wameweza kuzibadilisha kwa kujenga maziwa ya kutengeneza (*man-made lakes/reservoir*), vijito vidogo vidogo na mabwawa ambayo yameweza kuwa vivutio vikubwa vinavyochangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwenye nchi hizo. Sioni sababu kwanini hapa nchini hili lishindikane. Ni lazima tudhamirie, tuwe wabunifu zaidi na tutumie rasilimali tulizopewa na Mungu kujiletea maendeleo, huku tukizingatia matumizi bora na endelevu ya ardhi na utunzaji wa mazingira kwa faida ya kizazi hiki na vizazi vijavyo.

***Ndugu washiriki;***
Wiki iliyopita nilikuwa jijini Mbeya kuzindua Kampeni ya kupanda miti rafiki wa maji kwenye Vyanzo vyetu vyote vya maji na maeneo oevu hapa nchini. Vilevile mwezi Februari Mwaka huu nilizindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ambayo pamoja na mambo mengine inajumuisha utunzaji wa fukwe zetu. Nafahamu pia Taasisi nyingine ambazo si za kiserikali, zina programu mbalimbali za kupanda miti na kusafisha mazingira katika fukwe na maeneo mengine ya miji yetu. Hivyo, nina hakika tukiunganisha nguvu na kuboresha mikakati hususan ile inayohusu uchumi wa buluu, tutapata matokeo mazuri na tutafanikiwa kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Katika muktadha huu naagiza, kila Mkoa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, pamoja na wadau wengine kujipanga na kuharakisha mchakato wa kuandaa mpango mkakati utakaoainisha namna ya kufanya uwekezaji wa kuendeleza fukwe zilizopo (*beachfront development strategy*) au bustani za kupumzikia (*greenpark*

*development strategy)* kwa Mikoa isiyokuwa na fukwe na kuonesha tulivyojipanga kutekeleza. Mchanganyiko mzuri wa uhifadhi ukiambatana na huduma za kitalii, utaleta hamasa katika kuongeza utalii wa ndani na nje katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Ninaitaka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhakikisha kazi hii inakamilika hima na nipatiwe taarifa kamili ya mipango hii mapema iwezekanavyo.

Halikadhalika, ni matarajio yangu kuwa kongamano hili, liitajadili kwa kina na kuja na mapendekezo mazuri ya namna bora ya kuboresha mifumo yetu ya usimamizi, ulinzi na uwekezaji ili tuweze kutoka hapa tulipo. Serikali yenu ni sikivu na ipo tayari kupokea maoni yenu na kuyafanyia kazi kwa manufaa ya Taifa. Ninatarajia pia kuwa Taasisi ya UONGOZI itawasilisha taarifa nzuri ya majadiliano ya Kongamano hili mapema iwezekanavyo.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Washiriki, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

Napenda nihitimishe hotuba yangu kwa kuwakaribisha wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza katika fukwe zetu na sekta nyingine za kiuchumi katika nchi yetu. Tanzania ina utajiri mkubwa wa rasilimali na pia ni nchi yenye amani ambayo ni mtaji mkubwa kwa uwekezaji endelevu. Hivyo uwekezaji Tanzania, ni uwekezaji wa uhakika na wa kudumu!

Mwisho, napenda kuwashawishi washiriki wote wa Kongamano hili kutenga muda wa kutembelea maeneo yetu ya vivutio katika jiji la Mwanza na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria kama hifadhi za Rubondo, Burigi-Chato na hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Baada ya kusema hayo sasa **ninayo heshima kutamka kuwa Jukwaa la ukuaji wa kijani la mwaka 2022 limefunguliwa rasmi**. Nawatakia majadiliano mema.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**